

ZABUNI NA. CUHAS/01/2020/2021

UPANGISHAJI WA MAENEO YA HUDUMA YA CHAKULA

Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Sayansi za Afya (CUHAS) – Bugando kinawatangazia na kuwakaribisha kuleta maombi Wafanyabiashara/Kampuni/Taasisi/Watu Binafsi wenye uwezo wa kupanga maeneo ya huduma ya chakula yaliyopo Chuoni hapa kama ifuatavyo;

NA	NA. YA ENEO	UKUBWA WA ENEO
1	1	106 SqM
2	2	97.5 SqM
3	3	97.5 SqM
4	4	97.5 SqM
5	5	97.5 SqM

Kila eneo lina sehemu zifuatavyo:-

- (a) Chumba cha huduma ya chakula na Kaunta (Service Area)
- (b) Chumba cha kupikia
- (c) Stoo
- (d) Veranda nyuma ya chumba cha kupikia
- (e) Eneo la wazi nyuma ya chumba cha kupikia

Licha ya maeneo matano ya huduma ya chakula yanayopangishwa, liko eneo la jumla lenye uwezo wa kukalisha wateja zaidi ya 500 (mia tano) kwa wakati mmoja. Eneo lote hili limezekwa.

1. MASHARTI YA ZABUNI

- i. Mwombaji anapaswa kulipa ada ya maombi ya Zabuni ambayo ni Tshs 50,000/- kupitia ACCOUNT Namba. 01J105404045501, CUHAS – BUGANDO. **Ada hiyo haitarudishwa**
- ii. Mwombaji anapaswa kutaja kiasi atakacholipa CUHAS kama kodi ya pango kwa mwaka
- iii. Mwombaji awe na Leseni hai ya biashara ya chakula, Cheti cha Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN) pamoja na nakala ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kama ipo
- iv. Mwombaji anaweza kuomba kama Mtu Binafsi / Kikundi / Taasisi au Kampuni. Kama mwombaji ni Kampuni, Kikundi au Taasisi anapaswa kuambatanisha nakala ya Hati ya Usajili
- v. Mwombaji atakayeshinda atapaswa kukilipa CUHAS kodi ya miezi 12 kwa mara moja au kwa awamu mbili ndani ya siku saba tangu apewe barua ya tuzo
- vi. Mwombaji haruhusiwi kuomba chumba cha biashara zaidi ya kimoja
- vii. Gharama za maji na umeme zitalipwa na mpangaji mwenyewe
- viii. Mwombaji asiwe anadaiwa kodi na CUHAS, iwapo alikuwa mpangaji wa awali
- ix. Nyaraka za maombi ziwe na nakala halisi moja iliyofungwa kwa LAKIRI, iandikwe juu ya bahasha “NAMBA YA CHUMBA KINACHOOMBWA NA ZIKABIDHIWE KWENYE OFISI YA Katibu wa Bodi ya Zabuni, Ofisi namba 309, ghorofa ya tatu jengo la Utawala – CUHAS.
- x. Mzabuni anashauriwa kutembelea eneo analoomba kupanga kabla ya kujaza maombi ya zabuni
- xi. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi ya zabuni ni siku ya Ijumaa, tarehe 27/11/2020 kabla ya saa sita na nusu mchana (12:30). Zabuni zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa

kuwasilisha zabuni, waombaji wote au wawakilishi wao wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni hizo utakaofanyika siku hiyo katika ukumbi wa zamani wa mikutano (Old Boardroom) uliopo katika jengo la Utawala ghorofa ya tatu

- xii. Zabuni zitakazochelewa kuwasilishwa na Zabuni za kielektroniki hazitakubaliwa kwa tathmini
- xiii. CUHAS hakitalazimika kukubali/kutokukubali kutoa Zabuni kwa mwombaji yeyote kutokana na kigezo cha malipo makubwa/malipo kidogo ya Zabuni
- xiv. Maeneo yote matano ni kwa ajili ya huduma ya chakula na vinywaji baridi tu. Bidhaa nyingine zozote tofauti na hizi hazitaruhusiwa kuuzwa au kuhifadhiwa katika maeneo hayo. Vilevile matumizi ya kuni na Maranda hayataruhusiwa.
- xv. **Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo:**

**MAKAMU MKUU WA CHUO,
CHUO CHA KIKATOLIKI CHA SAYANSI ZA AFYA,
P.O.BOX 1464,
MWANZA.**